# DOYEN PUBLISHERS
## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## MTIHANI WA MWISHO MUHULA WA 1 2025
## GREDI YA 9 – KISWAHILI
*(Kartasi ya 2 - Insha na Utangulizi wa Fasihi)*

**Muda: Saa 1 dakika 45**

JINA: ______________________________________________________________

SHULE: _____________________________________________________________

KITENGO: _______________________ TAREHE: ___________________________

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

a) Andika jina lako, shule, kitengo na tarehe katika sehemu zilizo hapo juu.
b) Karatasi hii ina sehemu mbili; **A** na **B**.
c) Jibu maswali **yote**.
d) Andika majibu **yote** kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
e) Majibu **yote** ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**RUBRIKI YA TATHMINI**

| ALAMA (%) | NGAZI |
|---|---|
| **80 - 100** | Anazidi matarajio |
| **60 - 79** | Anafikia matarajio |
| **40 - 59** | Anakaribia matarajio |
| **0 - 39** | Chini ya matarajio |

**ALAMA ZA MWANAFUNZI**

| ALAMA | | JUMLA |
|---|---|---|
| Sehemu ya A (Kutoka kwa 15) | | |
| Sehemu ya B (Kutoka kwa 35) | | |

***Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa. Watahiniwa wanapaswa kukagua karatasi hii ili kuhakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa kama ilivyosemwa na hakuna maswali yanayokosekana.***

## SEHEMU A (Alama 15)

**INSHA**

**Maagizo:**

a) Chukua muda wa dakika **40** katika zoezi hili.
b) Andika insha yenye maneno kati ya **300 - 350** katika nafasi uliyoachiwa.

1. ***Anza kwa***: *Ufanisi wa mwanafunzi katika masomo humtegemea yeye*.................................................................

THE DOYEN PUBLISHERS EST 2023 L'AVENIR COMMENCE ICI

THE DOYEN PUBLISHERS
EST 2023
L'AVENIR COMMENCE ICI

## SEHEMU B (Alama 35)

**FASIHI SIMULIZI (Alama 10)**

2. ***Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Siku moja jioni, Paka mmoja alitembea kwenye mbuga kubwa ya kijiji akiwa na hamu ya kula. Alikuwa na njaa kali na alikuwa akitafuta kitu cha kumridhisha. Alipokuwa akitembea, aliona Panya mdogo akijificha nyuma ya jiwe. Alikuwa na woga akiona Paka akielekea upande wake, kwa sababu alikuwa anajua kwamba Paka ni mnyama mkali ambaye humshambulia kwa urahisi.

Paka alisimama mbele ya Panya na kusema kwa sauti ya upole, "Panya, siwezi kukufanya lolote kama utaniambia ukweli. Nimetafuta chakula kwa muda mrefu, lakini sijapata. Naona umekuwa na woga kwangu, lakini sitaki tena kuwa na uadui na wewe. Tumekuwa maadui kwa muda mrefu. Kwa nini tusijaribu kuwa marafiki?"

Panya alishtuka, lakini alijua kuwa Paka alikuwa na nguvu nyingi na alikuwa na uwezo wa kumkula. Hivyo alijua kuwa alikuwa na chaguo moja tu. Aliangalia Paka kwa macho ya shaka na kusema, "Paka, mimi ni mdogo na dhaifu. Sina nguvu wala spidi ya kukimbia kama wanyama wengine. Hata hivyo, mara nyingi mimi ni mwangalifu sana kwa sababu mimi ni mwepesi na siwezi kukubali kuwa urafiki wetu unakuwa na madhara. Ikiwa tutakuwa marafiki, je, utaendelea kuwa na njaa tu na kunifanya kuwa chakula chako?"

Paka alionekana kuchanganyikiwa lakini alijibu, "Hapana, Panya! Siwezi kumdhuru tena mtu yeyote. Nilikuwa na njaa tu, lakini sasa nadhani kuna njia nyingine. Tuwe marafiki na tusaidiane. Kama tutaishi kwa amani, huenda tutafaidika na umoja wetu."

Panya alifikiria kwa muda na akasema, "Sawa, tutajaribu. Lakini ukiona kuwa umeshindwa kuhimili njaa yako, tafadhali kumbuka kuwa mimi ni mdogo na siwezi kukupa chakula. Tujue mipaka yetu."

Hivyo basi, Paka na Panya walikubaliana kuwa marafiki na kuishi kwa amani. Walikuwa wakitembeleana mara kwa mara, wakizungumza na kucheka. Paka alijivunia kuwa na rafiki mdogo ambaye alimtambulisha kwa maeneo ya kijiji ambapo Panya alijua kila kona. Panya alifurahi kwa kuwa na rafiki ambaye alikuwa na nguvu za kumlinda kutokana na wanyama wakubwa waliokuwa na njaa.

Hata hivyo, kadri siku zilivyokuwa zikisonga, Paka alianza kuwa na njaa tena. Alijua kuwa Panya alikuwa mdogo na alikuwa na chakula kidogo, lakini aliona fursa ya kumshambulia. Alijua kuwa kama angeweza kumkamata Panya, angemla na kumaliza njaa yake.

Siku moja, Paka aliona Panya akicheza kwenye kivuli cha mti. Alijua kuwa alikuwa na fursa nzuri sasa. Alimzunguka kimyakimya na alijua kuwa ilikuwa ni wakati wake. Alimkaribia Panya kwa haraka na kumwambia kwa sauti ya nguvu, "Nataka kukuona kuwa chakula changu sasa. Umekuwa rafiki yangu kwa muda, lakini njaa yangu haijatosheka."

Panya aliguswa na maneno hayo, lakini aliweza kujua kwamba sasa ilikuwa ni wakati wa kukimbia. Alijua kuwa angetumia akili yake kuliko nguvu za mwili ili kuokoa maisha yake. Alianza kukimbia kwa kasi zaidi kuliko alivyowahi kufanya. Paka alijaribu kumshika, lakini Panya alikuwa mwepesi na aliweza kujificha kwenye shimo dogo.

Paka alikusanyika tena, akijua kuwa alijaribu kutumia rafiki yake kwa maslahi yake mwenyewe. Alijua kuwa Panya alikuwa na haki ya kuishi, na kwamba tabia yake ya dhuluma ilikuwa inaharibu uhusiano wao. Aliingia kwenye utambuzi wa kwamba kama kweli alitaka kuwa na amani na wengine, alipaswa kubadili tabia zake.

a) Hadithi hii ni ya aina ipi? Eleza. (alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b) Kwa nini Panya alikubali kuwa rafiki na Paka mwanzoni? (alama 2)

c) Eleza sifa **moja** ya paka katika hadith hii. (alama 2)

d) Eleza maadili tunayojifunza katika hadithi hii. (alama 4)

THE DOYEN PUBLISHERS EST 2023 L'AVENIR COMMENCE ICI

**NOVELA (Alama 10)**

3. ***Soma sehemu ifuatayo ya novela "Mshale wa Matumaini" na John Habwe kisha ujibu maswali.***

Mimi na wazazi wangu tulikuwa tukiishi Kisamale. Hapo ndipo palikuwa na mji wetu. Nilizaliwa hapo, nikakulia hapo hadi kujiunga na shule ya msingi. Udogoni nilikuwa nikitangamana na kila mtu bila kuwa na ubaguzi wa kimbari wala kikabila. Wakati huo niliamini kwamba binadamu wote tulikuwa sawa.

Muda ulisonga huku tukiendelea na shughuli zetu. Uvumi wa vurugu ulitulia kwa muda na maisha yakarejea hali yake ya kawaida. Binafsi nilishukuru sana. Nilikuwa na marafiki wengi Walanga na Wareba. Sikutaka kukosana nao. Ningekosana nao, ningecheza mpira na nani? Shuleni ningesoma vipi bila marafiki? Sikutaka mzozo baina yetu. Nilishukuru kuona kuwa amani ilirejea na watu waliendelea na shughuli zao za kawaida. Wakristo walienda makanisani na Waislamu wakaenda misikitini. Wanasiasa walifanya siasa zao na wakulima wakapanda mashambani mwao. Mavuno yalinawiri na kuvunwa. Jua lilichomoza mashariki na kutua magharibi. Kuku waliotaga mayai waliyaatamia na kuangua. Wa kunadi sala katika misikiti walinadi. Ndege wa mwituni waliimba. Upepo wa kusi ulivuma. Jua liliwaka na mvua kunyesha. Watu walizaliwa na wengine wakafa. Maji ya bahari yalijaa na kupwa. Siku zilisonga kama kawaida. Ghafla bin vuu, uvumi ulibisha hodi tena kwa kishindo. Mara hii ulikuwa na kishindo kikuu. Kila mtu aliyeusikia alifadhaika. Watu wengi walitapatapa kwa woga.

"Ala! Umerudi tena huu uvumi jamani," baba alimweleza mama jioni moja.
"Potelea mbali. Si kweli. Nikwambie mara ngapi ndipo unisikie? Hizo ni kelele za chura zisizomzuia tembo kunywa maji," mama alimwambia baba.

"Ninapendekeza mhamie Azania au Jamhuri ya Demokrasia ya Tereka kwa muda," baba alimshauri mama yangu.

"Sioni haja ya kuwa na wasiwasi namna hii. Habari hizi zitapita kama zilivyopita zile za awali," mama aliendelea kupinga ushauri wa baba.

a) Wahusika wakuu katika dondoo hili ni nani? (alama 2)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b) Kwa mtazamo wa mama, ni jinsi gani uvumi unavyoathiri jamii na watu binafsi? (alama 2)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c) Eleza mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika sehemu hii ya novela. (alama 4)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

d) Eleza maadili tunayojifunza kutoka kwa jinsi mama na baba wanavyoshughulikia uvumi katika familia yao? (alama 2)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**USHAIRI (Alama 5)**

5. ***Soma shairi lifuatalo kutoka Hodi Hodi Mashairi kisha ujibu maswali***

**Nimewakosea Nini?** ***(Mwalaa M. Nyanje)***

Wazazi baba na mama, nimewakosea nini?
Ndipo mkaona vyema, mkanitoa shuleni.
Mwaniachisha kusoma, sababu hasa ni nini?
Nimewakosea nini? Nimewakosea nini?

Wenzangu nikitazama, kila kucha wa mbioni,
Na mikoba yao nyuma, wamebeba migongoni.
Kati yetu nikipima, tofauti siioni.
Nimewakosea nini? Nimewakosea nini?

Karibu mwaka mzima, sijafika darasani,
Sioni mkijituma, kunirudisha shuleni.
Baba yangu kutwa nzima, anashinda ulevini.
Nimewakosea nini? Nimewakosea nini?

Mama naye pato zima, linaishia mwilini,
Kila nguo anapima, na vikoi kiunoni.
Ilhali nimekwama, mwaka mzima nyumbani.
Nimewakosea nini? Nimewakosea nini?

Sina njia ya kusema, yaliyo mwangu moyoni,
Moyoni yananiuma, nalia ndani kwa ndani.
Si neno bado mapema, nirudisheni shuleni.
Nimewakosea nini? Nimewakosea nini?

a) Malenga wa shairi hili ni nani? (alama 1)

b) Mbala na '**Nimewakosea nini?**' Lipe shairi hili vichwa vingine viwili. (alama 2)

c) Eleza muundo wa shairi hili kwa kuzingatia: ubeti, mishororo vipande na vina. (alama 4)

d) Kibwagizo cha shairi hili ni? (alama 2)

e) Ainisha mizani katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza. (alama 2)

f) Toja mfano wa inkisari katika shairi hili. (alama 2)

g) Eleza dhamira ya malenga katika shairi hili. (alama 2)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**



THE DOYEN PUBLISHERS EST 2023 L'AVENIR COMMENCE ICI